**Recent Books in Swahili (Tanzania) – May 2021**

**Mary Martin Booksellers Pte Ltd**
**Blk 231, Bain Street**
**#03-05, Bras Basah Complex**
**Singapore 180231**
**Tel : +65-6883-2284/6883-2204**
**info@marymartin.com**
**www.marymartin.com**

## Literature

Machozi Yamenishiya / Mohammed Khelef Ghassani
Dar es Salaam, Tanzania: Mkuki na Nyota Publishers Ltd, 2019
xxviii, 80p. ; 229x152mm.
9789987083756
$ 16.00 / PB
176gm.

Mateso, maumivu na siasa ni mambo yaliyojaa uchochezi mkali unaomsukuma mshairi kuzungumza waziwazi na kinagaubaga na hatimaye kumfanya mwandishi apandwe na jazba zinazofanya kazi fulani itoke nje ya kingo za ulingo wa kisanaa. Katika hali kama hii mshairi lazima atunge wimbo unaoimbika ndani ya nafsi yake mwenyewe kwanza, wimbo utakaomwezesha kunyanyuka kitandani asubuhi huku akijua hayuko pweke, ana wenzake wenye maumivu kama au kuliko yake. Mohammed Khelef Ghassani ana weledi huu wa kubaki ndani ya kingo za ulingo wa kisanaa, weledi wa kuichenga siasa kwa namna ya kuipa nguvu kubwa zinazoficha na kuzimua unagaubaga na hata ukali wake.
http://www.marymartin.com/web?pid=765535
---------------------------------------------------------------------------
Mwana Mdaga wa Mfalme (Le Petit Prince) / Antoine De Saint-Exupery (Translators) Philipp Kruse & Walter Bogya
Dar es Salaam, Tanzania: Mkuki na Nyota Publishers Ltd, 2011
108p. ; 210mmx155mm. ; Colour Illustrations

9789987080359
$ 25.00 / PB
134gm.

This is the first translation into Swahili of one of the classics of world literature, *Le Petit Prince*, first published in 1946 by Editions Gallimard in Paris. Since that time it has been translated into more than 190 languages and sold 80 million copies worldwide, and has been adapted for stage, screen and the opera. The author, Antoine de Saint-Exupery, drew on his experiences as an aviator in the Sahara desert. The narrator crashes in the Sahara where he meets the Prince and shows him his drawings, opening up the dialogue. The story moves to the little prince's asteroid/planet, from where he visits other asteroids each of which is inhabited by a foolish adult, and finally Earth. Through the conversations, observations of both humans, animals and the natural world, an extraordinary wisdom is imparted: a man who meets an extraordinary boy and relearns what it means to be a child; and a small boy learns of the wonders and ironies of life during the celestial odyssey. Together with the beautiful original illustrations, the timeless masterpiece opens a door for people of all ages to a new and deep philosophical understanding of life.
**http://www.marymartin.com/web?pid=212415**

--------------------------------------------------------------------------------

Mungu Hakopeshwi : Riwaya Hii Metunukiwa Tuzo Kiswahili Ya Mabati-Cornell Ya Fasihi Ya Afrika / Zainab Alwi Baharoon
Dar es Salaam, Tanzania: Mkuki na Nyota Publishers Ltd, 2017
258p. ; 198x129mm.
9789987753932
$ 17.00 / PB
290gm.

Riwaya ya Mungu Hakopeshwi inaelezea maisha ya familia moja ya Unguja iliyoingia katika mitafaruku na mikasa mingi. Kila kitu huwa na chanzo na khatima; basi ni nini chanzo cha

mitafaruku hiyo na khatima yake ilikuwaje? Simulizi ni juu ya baba, Bw. Ahmed, mwenye hasira kali zisizo na mipaka, aliyeongoza familia yake kwa utashi wa nafsi yake, bila kujali hisia za mkewe wala wanawe. Kumbe moyoni mwake alihifadhi siri, na hiyo siri ndiyo iliyomfanya Bw. Ahmed kuwa mkali bila kiasi, ikimsukuma azuie kurejea kwa yale yaliyomfika zamani. Lakini kivuli cha historia ya maisha yake ya nyuma hakikuacha kumuandama. Riwaya hii i meandikwa kwa lugha nzuri na fasaha, kwa ufundi wa msanii makini na mwelewa wa maisha ya jamii za Kizanzibari na za mwambao kwa jumla.
**http://www.marymartin.com/web?pid=765536**
**---------------------------------------------------------------------------**

Doa / Kithaka Wa Mberia
Nairobi, Kenya: Marimba Publications Limited, 2018
132p. ; 178x127mm.
9789966794420
$ 16.00 / PB
136gm.

Profesa Kithaka wa Mberia anafundisha na kufanya utafiti katika Idara ya Isimu na Lugha, Chuo Kikuu cha Nairobi, Nairobi, Kenya. Mbali na kufundisha na kufanya utafiti, anajishughulisha na uandishi wa mashairi na tamthilia. Tamthilia yake maarufu iitwayo Kifo Kisimani ilikuwa kitabu cha lazima katika mtihani wa kidato cha nne nchini Kenya kuanzia 2006 hadi 2012. Tamthilia yake nyingine iitwayo Natala ilikuwa kitabu cha kutahiniwa katika vyuo vya walimu, pia nchini Kenya, kuanzia 2005 hadi 2016. Mwandishi amewahi kukariri mashairi yake katika maeneo kadhaa ikiwa ni pamoja na Kenya, Tanzania, Iran, Marekani, US Virgin Islands, United Arab Emirates, Upolanzi, Ujerumani na Italia. Mbali na Doa, Kifo Kisimani na Natala, Profesa Kithaka wa Mberia amechapisha vitabu vingine ambavyo ni Mchezo wa Karata (mashairi), Bara Jingine (mashairi), Redio na Mwezi (mashairi), Msimu wa Tisa (mashairi), Rangi ya Anga (mashairi)

na Maua Kwenye Jua la Asubuhi (tamthilia). Diwani nyingine zake mbili za mashairi, Mvumo wa Helikopta na Bustani ya Miungu (huenda vichwa hivi vikabadilkika), zinatarajiwa kuchapishwa mwaka huu na mwaka ujao mtawalia.
**http://www.marymartin.com/web?pid=765537**

------------------------------------------------------------------------------

Mmeza Fupa / Ali Hilal
Dar es Salaam, Tanzania:  Mkuki na Nyota Publishers Ltd, 2019
212p. ; 198x129mm.
9789987083794
$ 17.00 / PB

Riwaya ya Mmeza Fupa ni riwaya iliyoshinda an kupewa tuzo ya Mabati-Cornell ya Fasihi ya Afrika kwa mwaka 2017. Katika tangazo la ushindi wa riwaya hii jopo la majaji lilitoa sifa zifuatazo: Si mno mtu kukutana na riwaya ya Kiswahili ambayo mwandishi wake amejidhihirisha kuwa ni mbuji wa lugha fasaha na ya kisanii, inayotiririka kitabia kwa hiari yake, na bila ya kuonesha dalili zozote kwamba imelazimishwa. Wahusika wake wote wamebuniwa kwa ustadi, na kupewa kazi muwafaka za kuziwakilisha tanzu na matabaka mbalimbali ya jamii - pamoja na mikinzano na mazingira yao ya kihistoria, ya kisiasa,ya kisaikolojia, ya kitamaduni, ya kimjini au ya kijijini. Licha ya kwamba matukio ya riwaya hii yanatokea katika kisiwa cha kubuni, maswala yanayojadiliwa humu ni miongoni mwa yale maswala sugu yanayoendelea kulisumbua bara la Afrika kisiasa, kijamii na kiuchumi. Riwaya hii inatudhihirishia mandhari mapya ya utanzu huu wa Fasihi ya Kiswahili.
Uzito wa mivutano ya karne na migongano ya zama hubebwa migongoni mwa mwanadamu. Huchuana na wakati, katika kupapatuana na tsunami ya matendo ya mwanadamu. Ndivyo alivyoibuka Bi. Msiri kwenye joto la visasi, akaponea chupuchupu kumezwa na chatu-binadamu. Siku ya kuteketezwa kwa familia yake yeye alikuwa mtoni kufua. Aliporudi nyumbani alipokewa na simanzi nzito na rekecho la harufu ya damu. Hapo hapakumweka, huo ukawa mwanzo wa yeye kuwa mfungwa huru, akalimeza fupa ndani ya mapito ya

karne mbili zilizompitia utosini. Kwa kuwa kwake mgubia chumvi nyingi chini ya jua, aliyajua mengi yaliyotiwa kapuni wakati ule. Akaweza kuja kuyasimulia wakati mwengine kwa vijana wengine aliowaamini.
**http://www.marymartin.com/web?pid=765538**

------------------------------------------------------------------------------

Mwanangu Rudi Nyumbani / Dotto Rangimoto
Dar es Salaam, Tanzania:  Mkuki na Nyota Publishers Ltd, 2018
94p. ; 198x129mm.
9789987083749
$ 16.00 / PB

Wakizingatia historia ndefu ya uandishi katika lugha ya Kiswahili, majaji wa Tuzo ya Kiswahili ya Mabati-Cornell ya Fasihi ya Afrika wameeleza: Mashairi yaliyomo katika diwani hii yametumiliwa lugha iliyojaa taswira na majazanda yanayowakilisha vyema hisia zinazoelezwa katika dhamira mbalimbali. Mshairi amefaulu sana kuzitumia mbinu na miundo kadha wa kadha ili kuyajadili maswala yanayohusu hali na mazingira tafauti tafauti katika maisha ya binadamu. Anayazungumza maswala mazito mazito, lakini kwa namna ambayo hayamuelemei msomaji wake. Bali, badala yake, huwa yanamhimiza aendelee kuyasoma. Hata yale maswala makongwe, kwa mfano uhusiano baina ya wazazi na wana wao, yanajadiliwa kwa namna ya kuvutia na kuyafanya kama kwamba ndiyo mwanzo yanaanza kujadiliwa sasa. Dotto Rangimoto ni mtunzi stadi. Na diwani hii ni mchango mkubwa katika ushairi wa Kiswahili wa zama zetu hizi.
**http://www.marymartin.com/web?pid=765539**

------------------------------------------------------------------------------